JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA
SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO

PHONE No. 0765783530 P.O.BOX 324
KYELA

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI ……
S. L. P …….
…….

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO MWAKA 2022</u>

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano (**V)** katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya HGL/HKL/HGK. Shule ya Sekondari KAFUNDO ipo umbali wa km 20 kutoka kyela mjini. Usafiri wa basi kutoka Kyela mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Kyela Mjini, nauli ni Tsh. 1500/= tu hadi Ipinda Mjini. Kutoka Ipinda mjini unaweza kutembea kwa miguu au ukatumia pikipiki (Bodaboda) kwa Tsh 1,000/= hadi shule ya sekondari Kafundo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **13/06/2022.**
Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/06/2022.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1 SARE YA SHULE.

(i) Sketi mbili rangi ya **dark blue (blue nyeusi)** na **kijivu** kitambaa kizito. Mshono uwe rinda pana mbele na nyuma, ziwe ndefu sana (Ziguse viatu). Kitambaa kimeambatanishwa, tafadhali zingatia rangi na aina ya kitambaa.)
(ii) Mashati mawili meupe tetroni mikono mirefu yasiyobana au yasiwe mafupi
(iii) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi jozi mbili, **vyenye kamba** na visivyo na visigino virefu.
(iv) Soksi rangi nyeupe jozi mbili.
(v) Tai rangi inayoendana na sketi
(vi) Sweta mbili moja rangi ya kijivu na nyingine blue nyeusi (dark blue)
(vii) Tracksuit rangi ya bluu bahari(Light blue)
(viii) Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo.
(ix) T-shirt inapatikana shuleni
(x) Gauni la kazi (Out of school uniform) rangi ya bluu bahari (light blue) ndefu isiyobana. (Nguo za nyumbani haziruhusiwi)
(xi) Kwa Waislamu hijabu nyeupe zisizokuwa na urembo.

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE.

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= unaweza kulipa kiasi cha Tsh 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

b) Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi/mlezi mara mwanafunzi anaporipoti shuleni: -

1. Taaluma …….….Tsh. 20,000/=
2. Vibarua/wapishi…….…….. Tsh. 30 ,000/=
3. Kitambulisho na picha……..….Tsh. 6,000/=
4. Ukarabati wa Samani…….....Tsh. 20,000/=
5. Huduma ya kwanza …… …….…Tsh. 5,000/=
6. Mtihani wa kujipima (Mock)……Tsh. 20,000/=
7. Nembo ya shule…….Tsh. 2000/=
8. Tahadhari …….…… Tsh. 5,000/= (Haitarejeshwa)
9. Kukodisha kodoro kwa mwaka….Tsh 10,000/=

N:B: *Jumla ya Ada na michango yote ni Tsh **188,000/=** zilipwe kwenye akaunti ya shule. Tafadhali andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi kwenye **pay in slip** na kuwasilisha siku ya kuripoti shuleni.*

JINA LA AKAUNTI**:** **KAFUNDO SEKONDARY SCHOOL**
NAMBA YA A KAUNTI**:** **60901200036 NMB**

2.3 MAHITAJI MUHIMU MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.

(a) Mahitaji ya mwanafunzi.

(i) Mashuka mawili rangi ya bluu bahari (light blue)
(ii) Chandarua
(iii) Blanketi dogo au shuka zito kwa ajilia ya baridi
(iv) Nguo za ndani za kutosha na mahitaji muhimu ya wasichana
(v) Taulo moja, kanga au kitenge
(vi) Nguo ya kulalia (Night dress) moja
(vii) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

(b) Mahitaji ya Taaluma na vifaa vya usafi wa mazingira.

(i) Bunda moja la karatasi kwa mwaka (Ream A4)
(ii) Daftari kubwa Dazani moja (Counter books)
(iii) Kalamu za wino na risasi
(iv) Mkebe wenye vifaa na Rula
(v) Vitabu vya masomo ya tahasusi yake
(vi) Flat file moja (spring file)
(vii) Ndoo mbili, moja lita ishirini na ndogo ya lita kumi zenye mifuniko

(viii) Brash ngumu ya mpini mrefu moja, mopa moja, ufagio wa ndani mmoja (soft bloom) na wa nje mmoja (chelewa) (ix) Jembe moja lenye mpini, kwanja moja na panga moja.

NB: MWANAFUNZI AJE NA NAKALA YA MATOKEO YA KUHITIMU KIDATO CHA NNE (RESULT SLIP) NA BIMA YA AFYA, KAMA ANAYO.

3.0 MAADILI MEMA.

(a) Kila mwanafunzi wa shule hii anatakiwa:-

(i) Kufuata sheria zote na taratibu za shule

(ii) Kuwahi na kuheshimu walimu, wafanyakazi, viranja wa shule na Wageni.

(iii) Kusimama na kusalimu wakubwa / walimu wanapopita au kuongea nao

(iv) Kuheshimu wanafunzi wengine

(b) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila kibali.

(i) Chumba cha walimu.

(ii) Ofisi za shule.

(iii) Maabara.

(iv) Nyumba za walimu.

(c) Mwanafunzi awapo shuleni hatakiwi kufanya yafuatayo:- (i) Kuonesha kiburi, ubishi na fitina kwa yeyote

(ii) Kunywa pombe, kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya (iii) Kutukana au kutumia lugha chafu na matusi, au uchokozi wowote ule.

(iv) Kukatisha kwenye viunga.

(d) Mwanafunzi wakati wote anatakiwa kuwa safi kwa:-

(i) Kuvaa nguo vizuri, kutumbukiza shati ndani ya sketi

(ii) Kunyoa nywele vizuri na kuzichana. Mitindo au upara haviruhusiwi

(iii) Kutovaa mapambo kama vile mikufu, kofia au pete n.k.

(e) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

(i) Vilabu vya pombe

(ii) Majumba ya starehe

(iii) Nyumba za wageni (Guest house)

4.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

4.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(i). Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wote, na jamii kwa ujumla
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
(iii) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation time)
(iv) Kuwa makini katika kila shughuli za shule utakazopewa
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo utakayopewa

(vi) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa(Nguo za nuymbani haziruhusiwi)
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

4.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa shule.

(i) Wizi
(ii) Uasherati, ubakaji, ushoga, ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji bangi
(iii)Makosa ya jinai
(iv)Kupigana au kupiga
(v) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
(vi)Kudharau bendera ya Taifa
(vii) Kuolewa
(viii) Kupata ujauzito au kutoa mimba
(ix)Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule
(x) Kukataa adhabu kwa makusudi
(xi) Kutumia au kuwa na simu shuleni.

5.0 Mambo mengine muhimu.

(i) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. Pamoja na vielelezo vingine vya daktari kama unamatatizo ya kiafya.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

(iv) Cheti cha matokeo ya kidato cha nne (Result slip)

6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO
S. L. P. 324
KYELA

JENNY A. NOMBO

MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE

FOMU A

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

(THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER).

Name of pupil …….

Age …… Sex ……..

The above named has been examined in respect of

(a) STOOL ……

(b) URINE ……..

(c) CHEST …….

(d) BLOOD …….

(e) EYES ……

(f) EARS …….

(g) OTHER FINDINGS ……....

……

……

…….....

I am satisfied that the above named pupil is /is not fit to pursue further studies in any secondary school.

…….. ……

SIGNATURE DATE

…… ……..

DESIGNATION STATION

FOMU B

FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

(IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)

Mimi (taja jina lako kamili) ……. nimechaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu ya Sekondari kidato cha tano (**V) 2021** katika Shule ya Sekondari Kafundo. Najaza fomu hii kukubali kuchaguliwa kwangu kuendelea na masomo katika shule hii. Naahidi kuwa niwapo katika shule hii nitatii na kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa kipindi chote cha masomo yangu.

Pia naahidi kuwa, kwa muda wote ni wapo katika shule hii sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kama nitakiuka na kwenda tofauti na mkataba huu, naomba sheria kali zichukuliwe dhidi yangu yaani **kufukuzwa shuleni** na **kushtakiwa Mahakamani**.

Nakubali kuwa nimesoma na kuelewa yote katika fomu hii ya mkataba na ninaahidi kuwa nitatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule.

SAHIHI YA MWANAFUNZI ……

TAREHE ……..……

FOMU C

FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

(IJAZWE NA MZAZI / MLEZI MWENYEWE)

Mimi mzazi / mlezi (Jina kamili …….……. ambaye ni mzazi / mlezi wa (Jina kamili la mwanafunzi) ……. najaza fomu hii kukubali maelezo yaliyoandikwa hapo juu. Kwa kujaza fomu hii, naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo katika kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata mahitaji yote (yake binafsi na mahitaji ya shule) kwa muda wake wote wa masomo ya Elimu ya Sekondari akiwa Kafundo Sekondari.

Iwapo sitatimiza wajibu wangu, naahidi kuwa sheria zichukuliwe dhidi yangu.

SAHIHI YA MZAZI / MLEZI ……..…….

TAREHE ……...…

FOMU D

HABARI KUHUSU MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi (Jina hili ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)

   …….

2. Tarehe ya kuzaliwa: ……...……

3. Mahali alipozaliwa (Wilaya): ……...…….

4. Mahali anapoishi sasa (Wilaya): ……..

5. Jina la Baba / Mlezi: …….

6. Anuani ya Baba /Mlezi ……..……

7. Jina la Mama / Mlezi: ……

8. Dini ya Mwanafunzi: ……

9. Dini ya Baba / Mlezi: ……...……

10. Dini ya Mama / Mlezi: ……..

11. Kazi ya Baba / Mlezi: ……...…….

12. Namba ya simu ya mzazi/mlezi……..

13. Michezo atakayoshiriki shuleni ni: …….

    …….

    ……..

RANGI YA KITAMBAA CHA KIJIVU